Corewell Health™

# SERA
# Sera ya Kudai Madeni na Bili za Gharama Zinazolipwa na Mgonjwa

**Sera Hii Inatumika katika maeneo yafuatayo ya Corewell Health:**
Beaumont Corporate Shared Services, Beaumont Dearborn, Beaumont Farmington Hills, Beaumont Grosse Pointe, Beaumont Medical Group, Beaumont Pharmacy Solutions, Beaumont Royal Oak, Beaumont Taylor, Beaumont Trenton, Beaumont Troy, Beaumont Wayne, Post Acute Care (Beaumont) Corewell Health (Corporate), Big Rapids (Mecosta County Medical Center), Continuing Care, Corporate, Gerber Memorial (Newaygo County General Hospital Association), Ludington (Memorial Medical Center of West Michigan), Outpatient/Physician Practices, Pennock (Pennock Hospital), Reed City (Reed City Hospital Corporation), SH GR Hospitals (Spectrum Health Hospitals), SHMG, Spectrum Health Lakeland (Lakeland Community Hospital Watervliet; Lakeland Hospitals at Niles and St. Joseph Inc.), United/Kelsey (Spectrum Health United; Spectrum Health Kelsey Hospital), Zeeland (Zeeland Community Hospital)

| | |
|---|---|
| **Matumizi Yanakomea kwa:** | N/A |
| **Nambari ya Marejeleo:** | 13636 |
| **Nambari ya Toleo:** | 5 |
| **Tarehe ya Kutekelezwa:** | 01/11/2022 |
| **Eneo la Utendaji:** | Fedha, Kipindi cha Mapato |
| **Eneo la Idara:** | Fedha, Ufikiaji wa Mgonjwa, Huduma za Fedha za Mgonjwa (PFS) |

**Ilani ya Kutobagua:** Corewell Health na kampuni zake zote tanzu zinapaswa kutoa huduma bora za afya kwa watu wote, kwa mujibu wa sera yake. Corewell Health haitabagua kwa misingi ya mbari, rangi, asili ya kitaifa, uraia, jinsia, dini, umri, ulemavu, imani za kisiasa, mwelekeo wa ngono, hali ya ndoa au familia. Maamuzi ya kusajiliwa na matibabu yatalingana kimahususi na mahitaji ya kimatibabu ya mgonjwa na uwezo wa hospitali kutoa huduma za matibabu na za kiafya zinazohitajika. Hutakatazwa kujisajili wala kupata matibabu kwa misingi ya kabila, rangi, jinsia, ngono, mbari, asili ya nchi, dini, ulemavu, umri, hali ya HIV, hali ya uanajeshi, chanzo cha malipo ya huduma au kwa misingi mingine yoyote iliyopigwa marufuku na sheria za serikali, za jimbo au za kimaeneo. Wagonjwa watatibiwa kulingana na utambulisho wa jinsia yao. Aidha, maeneo yaliyoidhinishwa ya National Health Service Corps (“NHSC”) na Michigan State Loan Repayment Program (“MSLRP”) hayatabagua katika kutoa huduma kwa mtu binafsi (na hayatategemea ustahiki kwenye mpango) kwa msingi wa uwezo wa mtu wa kulipa, iwe malipo ya huduma hizo yatafanywa kupitia Medicare, Medicaid, au CHIP; na hayatabagua kwa misingi ya mbari, rangi, jinsia, asili ya nchi, ulemavu, dini, umri, mwelekeo wa ngono au utambulisho wa jinsia ya mtu.

## 1. Madhumuni

Kuhakikisha huduma yenye usawa na haki kwa Wagonjwa na Wadhamini wote walio na Gharama Zinazolipwa na Wagonjwa zinazodaiwa na Corewell Health au kampuni zake tanzu. Katika hali hii, Corewell Health haitachukua Hatua za Ziada za Ukusanyaji wa Madeni dhidi ya Wagonjwa na/au Wadhamini ili kupata malipo ya matibabu kabla ya kufanya Bidii ya Kutosha kubaini kama Mgonjwa au Mdhamini anastahiki kupata usaidizi chini ya Sera ya Ustahiki wa Kupokea Usaidizi wa Kifedha (FAP).

Corewell Health™

Sera hii inalenga kutimiza na malipo kwa Wagonjwa ambao wanastahiki kupata usaidizi kwa mujibu wa Sera ya Usaidizi wa Kifedha katika Hospitali masharti ya Kifungu cha 501(r)(6) cha Kanuni ya Mapato ya Ndani cha 1986, kadri kinavyobatilishwa, ambacho hutoa masharti fulani kwa Hospitali kuhusu shughuli za ukusanyaji wa madeni.

**2. Ufafafuzi**

2.1. Deni: Gharama Inayolipwa na Mgonjwa ambayo Corewell Health au mshirika anayeiwakilisha zimejaribu kudai, ambayo haijalipwa kikamilifu au kusajiliwa kwenye mpango wa malipo baada ya njia zote za kudai za ndani wa Corewell Health au mshirika anayeiwakilisha kutofaulu.

2.2. Hatua za Ziada za Kudai (“ECA”): Hatua kama hizo ni pamoja na hatua ya kisheria, kuhusisha mshahara wa mgonjwa na ripoti za kodi.

2.3. Mdhamini: Mtu ambaye anatoa hakikisho la malipo ya huduma za Mgonjwa katika Corewell Health.

2.4. Mgonjwa: Mtu ambaye anapokea huduma katika Corewell Health au mojawapo ya kampuni zake tanzu.

2.5. Gharama Inayolipwa na Mgonjwa: Gharama zozote ambazo zinapaswa kulipwa na Mgonjwa na/au Mdhamini. Hii inajumuisha gharama ambayo haijawekewa bima, malipo ya pamoja, makato, bima za pamoja, huduma ambazo hazina bima na gharama yoyote inayodaiwa baada ya bima kukatwa, inayopaswa kulipwa na Mgonjwa na/au Mdhamini.

Iwapo Mgonjwa ana bima ya Medicaid na analipia huduma ambazo hazilindwi kwa bima (yaani, dawa anazojipatia, elimu ya uzazi), Corewell Health itachukulia gharama hizo kuwa zinastahiki kwenye uamuzi wa usaidizi wa kifedha.

2.6. Mtoa Huduma Mwingine wa Kudai Madeni: Kampuni iliyopewa kandarasi ya kudai Deni la Gharama Zinazolipwa na Mgonjwa kwa niaba ya Corewell Health lakini hutekeleza shughuli kama hiyo ya kudai chini ya jina lake mahususi kwa kufuata kanuni na sheria za Jimbo na Serikali.

2.7. Kipindi cha Ombi: Kipindi ambacho Corewell Health inapaswa kukubali na kuchakata Ombi la usaidizi wa Kifedha (kama ilivyofafanuliwa katika FAP). Kipindi cha Ombi huanza tarehe ambayo taarifa ya kwanza ya bili ya matibabu baada ya kuondolewa kwenye hospitali hutolewa na huisha baada ya siku 240. (Katika hali fulani, jinsi kwa mujibu wa Sera hii, Corewell Health inaweza kutakiwa ikubali na kuchakata Ombi la Usaidizi wa Kifedha baada ya kuisha kwa Kipindi cha Ombi.)

2.8. Sera ya Usaidizi wa Kifedha (FAP): Sera ya Usaidizi wa Kifedha ya Corewell Health ambayo kila kampuni yake tanzu inafuata ili kutambua na kutoa usaidizi wa kifedha kwa Wagonjwa ambao wanahitaji kusaidiwa kulipa bili zao za hospitali.

2.9. Jitahada za Kutosha: Hatua ambazo ni lazima Corewell Health ichukue ili kubaini kama Mgonjwa na/au Mdhamini anastahiki kupata usaidizi wa kifedha kwa mujibu wa Sera ya Usaidizi wa Kifedha, kabla ya kuhusisha ECA zozote kupokea malipo ya matibabu kwa mujibu wa kanuni za Internal Revenue Service na U.S. Department of Treasury.

Corewell Health™

3. **Majukumu**
Sera ya Kudai Madeni na Bili za Gharama Zinazolipwa na Mgonjwa itatekelezwa kwa njia inayofaa iliyobainishwa na wafanyakazi wa Corewell Health kama ilivyoainishwa katika taratibu husika.

4. **Kutii**
Ukiukaji wa sera hii unaotokana na wafanyakazi wa Corewell Health unaweza kusababisha hatua za adhabu.

5. **Sera**

5.1. Corewell Health itashirikiana na Wagonjwa na/au Wadhamini na wahusika wengine walioidhinishwa ili kubaini na kutekeleza suluhu zinazofaa kwa Gharama Inayolipwa na Mgonjwa. Gharama zinazolipwa na Mgonjwa zitashughulikiwa kwa mujibu wa Sera hii.

5.1.1. Wagonjwa Wanaokufa - Rambirambi kwa familia ya Mgonjwa aliyekufa wakati wa maombolezi ni kipaumbele cha Corewell Health. Corewell Health itabaini na kushughulikia Gharama zote Zinazolipwa na Mgonjwa jinsi ilivyotajwa katika Utaratibu wa Gharama Zinazolipwa na Mgonjwa au Mdhamini Aliyekufa. Jinsi ilivyobainishwa katika utaratibu huu, Corewell Health itatumia rekodi za umma kuthibitisha tarehe ya kufa, kutathmini ustahiki wa kupata usaidizi wa kifedha, Medicaid, na inaweza kutathmini hatua ya kutuma ombi la dai dhidi ya hali ya aliyekufa.

5.1.2. Wagojwa Waliofilisika - Corewell Health hutii Kanuni ya Marekani kuhusu Kufilisika. Kwa hivyo, Corewell Health itabaini na kushughulikia Gharama Zinazolipwa na Wagonjwa waliofilisika jinsi ilivyotajwa katika Utaratibu wa Gharama Zinazolipwa na Wagonjwa Waliofilika. Shughuli za kudai na bili zitakoma baada ya kupokea arifa ya kufilisika kwa tarehe zote za huduma zinazohusishwa na ripoti ya kufilisika. Corewell Health na washirika wake wengine watafuatilia kesi za kufilisika hadi ripoti ya kufilisika ikamilike au itupiliwe mbali.

5.1.3. Wagonjwa Wanaohitaji Usaidizi wa Kifedha – Corewell Health ina chaguo za usaidizi wa kifedha kwa Wagonjwa wenye Gharama Zinazolipwa na Wagonjwa kwa mujibu wa FAP. Kifungu hiki kinabainisha hatua ambazo ni lazima zichukuliwe katika hali mbalimbali ili Corewell Health iwe imefanya Jitihada za Kutosha za kubaini iwapo Mgonjwa na/au Mdhamini anastahiki kupata usaidizi wa kifedha katika FAP na kabla ya Corewell Health ijuhusishe na ECA yoyote dhidi ya mhusika.

5.1.3.1. Wagonjwa na/au Wadhamini wataarifiwa kuhusu FAP kwa maandishi jinsi ilivyofafanuliwa katika taratibu husika. Corewell Health itakubali maombi ya usaidizi wa kifedha kwa kuzingatia jitihada zote za ndani za kudai malipo na kuhusishwa kwa Mtoa Huduma Mwingine wa Kudai Madeni katika Kipindi cha Ombi.

5.1.3.1.1. Kuwasilisha Ombi Kamili la Usaidizi wa Kifedha.

- Kama Mgonjwa na/au Mdhamini atawasilisha ombi kamili la usaidizi wa kifedha wakati wa Kipindi cha Ombi, Corewell Health:
    - Itasitisha hatua zote za ECA
    - Itatoa uamuzi kuhusu kama Mgonjwa anastahiki kupokea usaidizi wa kifedha na kuarifu Mgonjwa na/au Mdhamini katika maandishi kuhusu uamuzi wa kustahiki (ikijumuisha, panapohitajika, usaidizi ambao Mgonjwa anastahiki kupokea) na msingi wa uamuzi huu.
    - Kama Mgonjwa atabainshwa kuwa anastahiki kupokea usaidizi wa kifedha kwa matibabu, Corewell Health:
        - Itampa Mgonjwa na/au Mdhamini arifa kupitia maandishi inayoeleza kuwa Mgonjwa na/au Mdhamini anastahiki kupokea usaidizi kwa mujibu wa FAP;

Huluki zitarejelea Hati husika zilizo katika hati hii panapohitajika
Huenda machapisho ya hati hii hayazingatii tarehe na yanayapaswa kuchukuliwa kuwa yasiyodhibitiwa.

- Itamrejeshea Mgonjwa na/au Mdhamini pesa zozote ambazo amelipa kwa matibabu, ambazo zimezidi kiasi kilichobainishwa kuwa atajilipia kwa mujibu wa FAP, isipokuwa kiasi hicho cha ziada kiwe chini ya $5 (au kiasi kingine kama hicho kilichochapishwa katika Internal Revenue Bulletin);
- Itachukua hatua zozote zinazofaa ili kubatilisha hatua zozote za ECA zilizochukuliwa dhidi ya Mgonjwa na/au Mdhamini ili kupata malipo ya matibabu.

5.1.3.1.2. Kuwasilisha Ombi Lisilokamilika la Usaidizi wa Kifedha

- Kama Mgonjwa na/au Mdhamini atawasilisha ombi lisilokamilika la usaidizi wa kifedha katika Kipindi cha Ombi, Corewell Health:
  - Itasimamisha kwa muda ECA kupata malipo ya matibabu.
  - Itampa Mgonjwa na/au Mdhamini notisi iliyoandikwa ambayo inafafanua maelezo ya ziada na/au hati zinazohitajika kwa mujibu wa FAP au fomu ya ombi la usaidizi wa kifedha ambayo lazima iwasilishwe ili kukamilisha ombi na maelezo kama hayo na/au hati lazima zipokelewe ndani ya siku thelathini (30) kuanzia tarehe ambapo notisi ya maandishi, au ombi litakataliwa na shughuli ya kudai malipo itaendelea.
    - Notisi hii itajumuisha maelezo ya mawasiliano ya Corewell Health.
  - Kama maelezo na/au hati za ziada zitapokelewa na akaunti iko katika Kipindi cha Ombi, akaunti hiyo itazingatiwa tena kwa usaidizi wa kifedha na shughuli za kudai malipo zitasitishwa hadi uamuzi utolewe.

5.1.3.1.3. Kutowasilisha Ombi la Usadizi wa Kifedha.

- Iwapo hakuna ombi la usaidizi wa kifedha lililotumwa katika Kipindi cha Ombi, Corewell Health inaweza kuanzisha hatua za ECA ili kupata malipo ya matibabu baada ya kumwarifu Mgonjwa na/au Mdhamini kuhusu FAP jinsi ilivyotajwa hapa ndani.

5.1.4. Marekebisho kwa Wagonjwa Wasio na Bima – Licha ya chochote kinachokinzana na sera hii, kwa huduma za hospitali zilizotolewa kwa Wagonjwa wasio na bima ambao malipo yao ya mwaka ni chini au sawa na 250% ya Mwongozo wa Marekani wa Kubaini Umaskini (FPG) na ambao hawastahiki kupokea FAP, Corewell Health itarekebisha gharama zozote za huduma kama hizo kuwa chini ya 115% ya viwango vya Medicare kwa huduma sawa au zinazolingana. Malipo ya gharama zilizorekebishwa yatazingatiwa kuwa malipo kamili ya huduma.

5.1.5. Chaguo za Malipo – Corewell Health itafafanua na kutoa chaguo za malipo kwa Mgonjwa na/au Mdhamini aliye na Gharama Inayolipwa na Mgonjwa ili kumwezesha Mgonjwa na/au Mdhamini kulipia gharama zao jinsi ilivyobainishwa katika Utaratibu wa Chaguo za Malipo ya Gharama Zinazolipwa na Mgonjwa. Malipo yote kwa njia ya pesa taslimu, hundi, Money Order au kadi ya mikopo. Chaguo nyingine za malipo zinajumuisha mipango ya malipo iliyopanuliwa ya nje au ndani.

5.1.6. Kudai Malipo - Iwapo Gharama Zinazolipwa na Mgonjwa bado hazijalipwa baada ya chaguo zote zilizobainishwa katika sehemu za 5.1.3.-5.1.5. hapo juu kuisha, Corewell Health inaweza kuwasilisha Gharama Inayolipwa na Mgonjwa kwa Mtoa Huduma Mwingine wa kudai Malipo, jinsi ilivyobainishwa katika Utaratibu wa Kudai Malipo na Bili za Gharama Zinazolipwa na Mgonjwa. Angalau taarifa nne (4)

za bili zitakuwa zimetumwa kwa Mgonjwa na/au Mdhamini, ndani ya siku 120, kabla ya kuwasilishwa.

5.1.6.1. Corewell Health itaidhinisha ECA zozote zifanyike ndani ya siku thelathini (30) za kwanza baada ya kuwasilishwa kwa Mtoa Huduma Mwingine wa Kudai Malipo.

5.1.6.2. Corewell Health haitajihusisha na ECA yoyote dhidi ya Mgonjwa na/au Mdhamini bila kufanya Jitihada za Kutosha ili kubaini ustahiki wa Mgonjwa katika FAP. Hasa, kama Corewell Health inapanga kufuatilia ECA, mambo yafuatayo yatafanyika angalau siku thelathini (30) kabla ya kuhusisha ECA mmoja au zaidi:

- Corewell Health itamwarifu Mgonjwa na/au mdhamini kwa maandishi kuwa usaidizi wa kifedha unapatikana kwa watu wanaostahiki na itabainisha ECA ambao Corewell Health (au Mtoa Huduma Mwingine wa Kudai Malipo) inapanga kuhusisha ili kupata malipo.
- Corewell Health itafanya Jitihada za kutosha ili kumwarifu Mgonjwa kuhusu FAP na jinsi Mgonjwa na/au Mdhamini anaweza kupata usaidizi kupitia mchakato wa kutuma ombi.

5.1.7. Majibu ya Barua - Majibu ya barua huchakatwa kwa kutumia hifadhidata ya USPS na masahihisho hufanywa inavyofaa. Ni wajibu wa Mdhamini kutoa anwani ya sasa ya kutuma barua wakati wa huduma au baada ya kuhama. Iwapo akaunti haina anwani sahihi, Corewell Health itachukulia kuwa Jitihada za Kutosha zimefanyika.

## 6. Mamlaka ya Mwisho

Mamlaka ya mwisho ya kuamua kama Corewell Health imefanya Jitihada za Kutosha ili kubaini kama Mgonjwa anastahiki kupokea usaidizi kwa mujibu wa FAP na yanayoweza kuhusisha ECA dhidi ya Mgonjwa na/au Mdhamini huwa ni Makamu Mkuu wa Rais, Revenue Cycle au mwakilishi wake.

## 7. Marekebisho

Corewell Health inahifadhi haki ya kubadilisha, kubatilisha, kugeuza au kuondoa sera hii wakati wowote bila ilani ya awali iliyoandikwa.

## 8. Marejeleo

Sera ya Ustahiki wa Usaidizi wa Kifedha
Utaratibu wa Gharama Zinazolipwa na Mgonjwa au Mdhamini Aliyekufa
Utaratibu wa Gharama Zinazolipwa na Mgonjwa Aliyefilisika
Utaratibu wa Chaguo za Malipo ya Gharama Zinazolipwa na Mgonjwa - PFS

## 9. Kubuni na Kuidhinisha Sera

**Mmiliki wa Hati:**
Paula Cersosimo (Administrative Assistant)

**Mwaandishi (Waandishi):**
Crystal Lang (Mgr, Patient Financial Services)

**Mkaguzi (Wakaguzi):**
Amy Assenmacher (SVP, Finance Revenue Cycle), Courtney Guernsey (VP, Patient Financial Services), Matthew Cox (Chief Financial Officer), Sarah Clark (VP, Registration/Fin Counseling), Steffany Dunker (Managing Counsel)

**Mwidhinishaji:**
Christina Freese Decker (President & CEO)

# Kiambatisho cha A

**Ilani ya Kutobagua:**
Kwa kujibu wa sera ya Corewell Health na kampuni zake zote tanzu, zinapaswa kutoa huduma bora za afya kwa watu wote. Maamuzi ya kusajiliwa na matibabu yatalingana kimahususi na mahitaji ya kimatibabu ya mgonjwa na uwezo wa hospitali kutoa huduma za matibabu na za kiafya zinazohitajika. Hutakatazwa kujisajili wala kupata matibabu kwa misingi ya kabila, rangi, jinsia, ngono, mbari, asili ya nchi, dini, ulemavu, umri, hali ya HIV, hali ya uanajeshi, chanzo cha malipo ya huduma au kwa misingi mingine yoyote iliyopigwa marufuku na sheria za serikali, za jimbo au za kimaeneo. Wagonjwa watatibiwa kulingana na utambulisho wa jinsia yao. Maeneo yaliyoidhinishwa ya NHSC yanapaswa kukubali kutobagua katika utoaji wa huduma kwa watu kulingana na: hali ya mtu kutoweza kulipia huduma; iwe malipo ya huduma hizo yatafanywa kupitia Medicare, Medicaid, au CHIP; kabila, rangi, jinsia, asili ya nchi, ulemavu, dini, umri, mwelekeo wa kingono au utambulisho wa kijinsia.

Angalia sera ya [Haki na Wajibu wa Mteja](#) kwa maelezo zaidi

Corewell Health:

- Hutoa huduma na misaada bila malipo kwa watu walio na ulemavu ili wawasiliane ipasavyo nasi, kama vile:
  - Wakalimani waliohitimu wa lugha ya ishara
  - Maelezo yaliyoandikwa katika miundo mingine (maandishi makubwa, sauti, miundo ya kielektroniki inayoweza kufikiwa, miundo mingine)
- Hutoa huduma za lugha bila malipo kwa watu ambao lugha yao msingi si Kiingereza, kama vile:
  - Wakalimani waliohitimu
  - Maelezo yaliyoandikwa kwa lugha nyingine

Iwapo unahitaji huduma hizi, wasiliana na Corewell Health Language Services katika: 616.267.9701 au 1.844.359.1607 (TTY:711)

Iwapo unaamini kuwa Corewell Health imeshindwa kutoa huduma hizi au imebagua kwa njia nyingine kwa misingi ya mbari, rangi, nchi asili, umri, ulemavu, au jinsia, unaweza kutuma malalamiko kupitia:

- Kwa Legacy Beaumont Health:
  Patient Experience Department
  26901 Beaumont Blvd
  Southfield, MI 48033
  947-522-1472
  Pfcc@beaumont.org

- Kwa Legacy Spectrum Health Lakeland na Legacy Spectrum Health West Michigan:
  Director, Patient Experience
  100 Michigan St NE, MC 006
  Grand Rapids, MI 49503
  616-391-2624; bila malipo: 1-855-613-2262
  Patient.relations@spectrumhealth.org

Unaweza kuwasilisha malalamiko ana kwa ana au kupitia barua ya posta, au barua pepe. Iwapo unahitaji usaidizi wa kuwasilisha malalamiko, Msimamizi wa Huduma za Wagonjwa anaweza kukusaidia.

Unaweza pia kuwasilisha malalamiko ya haki za raia kwa U.S. Department of Health and Human Services, Office for Civil Rights kwa njia ya kielektroniki kupitia Office for Civil Rights Complaint Portal, inayopatikana katika https://ocrportal.hhs.gov/ocr/portal/lobby.jsf, au kupitia barua pepe au simu kwa:

U.S. Department of Health and Human Services
200 Independence Avenue SW, Room 509F, HHH Building
Washington, DC 20201
1-800-368-1019, 800-537-7697 (TDD).

Fomu za malalamiko zinapatikana katika http://www.hhs.gov/ocr/office/file/index.html.

**Wasiliana Nasi**

**Español (Spanish)**
ATENCIÓN: Si usted habla español, tiene a su disposición servicios gratuitos de asistencia lingüística. Llame al 1-844-359-1607 (TTY: 711).

**العربية (Arabic)**
ملحوظة: إذا كنت تتحدث اللغة العربية، فإن خدمات المساعدة اللغوية تتوافر لك بالمجان. اتصل برقم 1-844-359-1607 (رقم هاتف الصم والبكم: 711).

**中文 (Chinese): 國語/普通話 (Mandarin), 粵語 (Cantonese)**
請注意：如果您講中文，你可以獲得免費的語言輔助服務。請撥打1-844-359-1607（TTY 手語翻譯：711）。

**Tiếng Việt (Vietnamese)**
CHÚ Ý: Nếu bạn nói Tiếng Việt, có các dịch vụ hỗ trợ ngôn ngữ miễn phí dành cho bạn. Gọi số 1-844-359-1607 (TTY: 711).

**Ako govorite srpsko (Serbian, Croatian or Bosnian)**
OBAVJEŠTENJE: Ako govorite srpsko-hrvatski, usluge jezičke pomoći dostupne su vam besplatno. Nazovite 1-844-359-1607 (TTY: 711). (TTY- Telefon za osobe sa oštećenim govorom ili sluhom: 711).

**አማርኛ (Amharic)**
ማስታወሻ: የሚናገሩት ቋንቋ ኣማርኛ ከሆነ የትርጉም እርዳታ ድርጅቶች፣ በነጻ ሊያግዝዎት ተዘጋጀተዋል፡ ወደ ሚከተለው ቁጥር ይደውሉ 1-844-359-1607. (መስማት ለተሳናቸው: (TTY: 711).

**नेपाली (Nepali)**
ध्यान दिनुहोस्: तपाईंले नेपाली बोल्नुहुन्छ भने तपाईंको निम्ति भाषा सहायता सेवाहरू निःशुल्क रूपमा उपलब्ध छ । फोन गर्नुहोस् 1-844-359-1607 (टिटिवाइ: (TTY: 711).

**Thuɔŋjaŋ (Nilotic – Dinka)**
PIĐ KENE: Na ye jam në Thuɔŋjaŋ, ke kuɔny yenë kɔc waar thook atö kuka lëu yök abac ke cïn wënh cuatë piny. Yuɔpë 1-844-359-1607 (TTY: 711).

**Kiswahili (Swahili)**
KUMBUKA: Ikiwa unazungumza Kiswahili, unaweza kupata, huduma za lugha, bila malipo. Piga simu 1-844-359-1607 (TTY: 711).

**فارسی (Farsi)**
توجه: اگر به زبان فارسی گفتگو می کنید، تسهیلات زبانی بصورت رایگان برای شما فراهم می باشد. با 1.844-359-1607 (TTY: 711). تماس بگیرید.

**Français (French)**
ATTENTION: Si vous parlez français, des services d'aide linguistique-vous sont proposés gratuitement. Appelez le 1.844-359-1607 (TTY: 711).

**မြန်မာ (Burmese)**
သတိပြုရန်- သင် မြန်မာစကားပြောဆိုပါက ဘာသာစကား အကူအညီဝန်ဆောင်မှုများကို အခမဲ့ ရရှိနိုင်ပါသည်။ 1-844-359-1607, (TTY: 711) ကို ခေါ်ဆိုပါ။

Corewell Health™

**(Dari) فارسی دری**

توجه اگر به زبان دری صحبت می کنید، خدمات کمک زبانی بصورت رایگان برای شما در دسترس است. تماس 1-844-359-1607 (TTY: 711).
ب

**Kreyòl Ayisyen (Haitian Creole)**
ATANSYON: Si ou pale Kreyòl Ayisyen, gen èd nan lang ki disponib gratis pou ou. Rele nimewo 1-844-359-1607 (TTY: 711).

**Ikinyarwanda (Kinyarwanda)**
ICYITONDERWA: Niba uvuga ikinyarwanda, serivisi z'ubufasha ku byerekeye ururimi, urazihabwa, ku buntu. Hamagara 1-844-359-1607 (ABAFITE UBUMUGA BW'AMATWI BIFASHISHA ICYUMA CYANDIKA -TTY: 711).

**Soomaali (Somali)**
DIGTOONI: Haddii aad hadasho Soomaali, adeegyada caawimada luqadda, oo bilaasha, ayaad heli kartaa. Wac 1.844-359-1607 (TTY: 711).

**(Sudanese) اللهجة السودانية**

انتباه: إذا كنت تتحدّث اللهجة السودانية، خدمات المساعدة بلغتك متاحة مجاناً. اتصل على الأرقام 1-844-359-1607 (رقم الصم والبكم: 711).

**தமிழ் (Tamil)**
கவனம்: நீங்கள் தமிழ் பேசினால், உங்களுக்கு இலவசமான மொழி உதவிச் சேவைகள் கிடைக்கின்றன.இந்த எண்ணை அழைக்கவும்: 1-844-359-1607 (TTY: 711).

**ትግርኛ (Tigrinya)**
ትኹረት: ትግርኛ እንድሕር ትዛረብ ኮንካ፣ ናይ ቋንቋ ደገፍ ኣልግሎታት፣ ብናጻ ክቐርቡልካ እዮም። ደውል 1.844-359-1607 (TTY: 711)።

)
ATANSYON: Si ou pale Kreyòl Ayisyen, gen èd nan lang ki disponib gratis pou ou. Rele nimewo 1-844-359-1607 (TTY: 711).

**Ikinyarwanda (*Kinyarwanda*)**
ICYITONDERWA: Niba uvuga ikinyarwanda, serivisi z'ubufasha ku byerekeye ururimi, urazihabwa, ku buntu. Hamagara 1-844-359-1607 (ABAFITE UBUMUGA BW'AMATWI BIFASHISHA ICYUMA CYANDIKA -TTY: 711).

Soomaali (***Somali***)
DIGTOONI: Haddii aad hadasho Soomaali, adeegyada caawimada luqadda, oo bilaasha, ayaad heli kartaa. Wac 1.844-359-1607 (TTY: 711).

**Sudanese**اللهجة السودانية (
**انتباه: إذا كنت تتحدّث اللهجة السودانية، خدمات المساعدة بلغتك متاحة مجاناً. اتصل على الأرقام**
. 1607-359-844-1)711: رقم الصم والبكم)
தமிழ் (***Tamil***)
கவனம்: நீங்கள் தமிழ் பேசினால், உங்களுக்கு இலவசமான மொழி உதவிச் சேவைகள் கிடைக்கின்றன.இந்த எண்ணை அழைக்கவும்: 1-844-359-1607 (TTY: 711).

ትግርኛ (***Tigrinya***)
ትኹረት: ትግርኛ እንድሕር ትዛረብ ኮንካ፣ ናይ ቋንቋ ደገፍ ኣልግሎታት፣ ብናጻ ክቐርቡልካ እዮም። ደውል 1.844-359-1607 (TTY: 711)።